**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1358
*Utathmini wa Vitendoneni katika Ngano za Kinyankole*

# Utathmini wa Vitendoneni katika Ngano za Kinyankole

**Benon Mukundane[1], Magdaline Wafula[1] & Nathan Ogechi[2]**
[1]*Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu cha Kisii, Kenya*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-03-24
Kurekebishwa: 2025-09-22
Kukubaliwa: 2025-09-30
Kuchapishwa: 2025-10-15

**Maneno Muhimu**
Kuitikia
Kujamiisha
Usimulizi-tendi
Vitendoneni

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Mukundane, B., Wafula, M., & Ogechi, N. (2025). Utathmini wa Vitendoneni katika Ngano za Kinyankole. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(2), 55-65.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii inabainisha vitendoneni katika ngano za Kinyankole na athari za vitendoneni hivyo kwa wasikilizaji. Wanyankole wa jadi walizoea kusimuliana ngano na usimulizi wao ulitumia vitendoneni ambavyo viliathiri hadhira na kuichochea kutenda. Hata hivyo, vitendoneni hivi vilikuwa havijabainika. Makala hii, kwa hiyo, inabainisha, inachanganua na inawasilisha vitendoneni vinavyojitokeza katika ngano za Kinyankole na jinsi vinaathiri hadhira. Uchambuzi wa vitendoneni hivi umeongozwa na nadharia ya Kitendoneni ya Austin (1962). Data ya utafiti imekusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na uchunguzi shirikishi na imetoka kwa watafitiwa 36 ambao tumewateua kimaksudi. Kutoka kwa ngano ishirini tulizokusanya nyanjani, tumechambua ngano saba ambazo tumeteua kinasibu. Uchanganuzi wa data umejikita kwa mkabala wa kiethnografia wa muundo wa kithamano ambao unawasilisha data kiufafanuzi na kimaelezo. Utafiti umegundua kuwa usimulizi wa ngano za Kinyankole unatumia mitindo kisanaa na mitindo hiyo inatumia vitendoneni vinavyoathiri wasikilizaji na kuwachochea kuitikia kwa kutekeleza majukumu mbalimbali. Vitendoneni ambavyo vimebainika ni vya maamuzi, vya maagizo, maagano, maelezo, hisia na vya hulka. Vitendoneni hivi vinaathiri wasikilizaji kwa njia chanya na kwa njia hasi. Kichanya, vinachochea hadhira kutekeleza majukumu kama vile kufanya kazi kwa bidii na kuendeleza maadili ya kitamaduni. Kihasi, vinaibua mihemuko, huzuni, chuki na hamu ya kulipiza kisasi. Makala hii imehitimisha kwamba vitendoneni vinavyotumiwa katika usimulizi wa ngano za Kinyankole vinachangia uimarishaji wa maadili na utekelezaji majukumu fulani.

## Utangulizi

Wanyankole wanaishi Magharibi ya Kusini mwa Uganda katika jimbo la Ankole. Lugha ya Wanyankole ni Kinyankole. Ninsiima (2021) anadai kwamba Wanyankole wamekuwa wakitumia lugha yao kuendeleza utamaduni wao kutoka kizazi hadi kingine. Jamii ya Wanyankole ilikuwa na amali ambazo ziliitambulisha, kwa mfano, usimulizi wa ngano, nyimbo za kitamaduni, mavazi, vyakula, vitendawili na methali, miongoni mwa nyingine (Kyobutungi, 2012). Amali hizi zilikuwa nyenzo kuu ya kukijamiisha kizazi kichanga na kwa njia hii kuhifadhi utambulisho wa jamii, (Kirindi, 2008). Kulingana na Kirindi, (keshatajwa), amali za kitamaduni za Kinyankole zimekuwa zikipitishwa kwa njia ya mdomo na zilichangia kufunza vijana kuhusu jamii yao na pia kutambulisha wanajamii kwa ujumla. Nganwa (1962) anasema jamii nyingi za Kiafrika zilitumia fasihi simulizi kufunza maadili kwa watoto wao. Anataja ngano kama aina ya fasihi simulizi

ambayo ilitumiwa kuadilisha jamii. Wazee hasa ndio waliwasimulia vijana ngano wakati wa jioni (Insaidoo, 2011; Okpewho, 1986; Finnegan, 1974; Mushanga, 1969). Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii ambazo zilitumia ngano kukuza na kuendeleza maadili miongoni mwa vijana. Usimulizi wa ngano za Kinyankole ulitumia vitendoneni ambavyo viliathiri wasikilizaji na kuwachochea kuitikia kwa kutenda majukumu mbalimbali.

Licha ya majukumu ambayo ngano za Kinyankole zilitenda, zinaelekea kudidimia kutokana na athari za usasa ambazo zinaendelea kudidimiza fasihi simulizi za Kiafrika, mkiwemo usimulizi wa ngano. Athari hizi zimeletwa na mifumo migeni ya elimu na dini ambayo imeshinikizwa na wimbi la utandawazi. Zaidi ya hayo, maendeleo ya sayansi na teknolojia yanatishia umaarufu wa fasihi simulizi. Baadhi ya Wanyankole wa kizazi kichanga hawatapata fursa ya kufundishwa kupitia mfumo wa fasihi simulizi na huenda wasiithamini turathi hii adimu na hatimaye kuipoteza iwapo jitihada za dharura hazitachukuliwa kuwaelimisha. Athari ya kudidimia kwa usimulizi wa ngano za Kinyankole ni kwamba, vijana watapoteza maarifa na mafunzo yaliyofunzwa na ngano za Kinyankole. Aidha, hawatajifunza mitindo ya usimulizi iliyotumiwa na watakosa mafunzo kama yalivyoendelezwa na vitendoneni vilivyojitokeza katika usimulizi wa ngano.

**Mabadiliko katika Usimulizi wa Ngano za Kinyankole**

Wanyankole wa jadi walienzi sana usimulizi wa ngano za Kinyankole (Mushanga, 1969). Usimulizi wa ngano zao ulitumia mitindo kisanaa na mitindo hiyo ilinata hamu ya wasikilizaji. Pia iliburudisha hadhira na kurahisisha uelewa wa ujumbe. Kwa njia hii, hadhira iliburudika na wakati huo huo ikapata mafunzo. Kirindi (2008) anatambua kuwa kusimulia ngano kwa ustadi kulikuwa kipawa ambacho kilienziwa sana na Wanyankole wa jadi. Usimulizi wa ngano ulichukuliwa kuwa njia mojawapo kuu ya kufunzia vijana kuhusu maadili ya utamaduni wao. Wazazi na wazee walitumia ngano kuwahimiza vijana kuwajibikia majukumu maalum kama yalivyotarajiwa katika jamii yao.

Kwa sasa, kumeendelea kuwa na mabadiliko kutokana na mifumo ya kigeni ya elimu ambayo inashinikizwa na wimbi la utandawazi kote ulimwenguni. Mazingira ya kijamii yaliyowapa wazazi, mababu na mabibi kutangamana kila siku hayapo tena. Hali hii imeathiri fani ya usimulizi wa ngano katika jamii nyingi za Kiafrika, jamii ya Wanyankole ikiwemo. Maarifa ya usimulizi wa ngano yaliyopokezwa kutoka kizazi hadi kingine yanaanza kupotea na nafasi yake kuchukuliwa na vifaa vya kisasa kama maandishi, video na vibonzo kwenye redio, runinga na mitandaoni.

Baadhi ya uhondo uliosheheniwa na usimulizi wa ngano za Kinyankole ni matumizi ya vitendoneni ambavyo viliacha athari ya kudumu kwa hadhira. Hadhira iliathirika ama kihasi au kichanya lakini kwa vyovyote vile, jamii iliishia kubadilika kitabia. Athari hizi zilichochea hadhira kutenda vitendo mbalimbali kulingana na jinsi waliathirika. Kwa hivyo vitendoneni katika ngano vinakuwa na nguvu za kubadilisha mienendo ya wanajamii na kuimarisha utangamano na mshikamano wa kijamii. Makala hii inavijadili vitendoneni vilivyojitokeza katika ngano mahsusi za Kinyankole zilizosimuliwa nyanjani na athari mahsusi zilizojitokeza kwa hadhira lengwa.

**Misingi ya Kinadharia**

Uchanganuzi wa data katika makala hii uliongozwa na nadharia ya Kitendoneni. Kitendoneni ni utoaji wa matamko ambayo husababisha utendaji wa tendo (Mahmoud, 2018). Matinde (2012) anadai kuwa kitendoneni ni tamko ambalo husababisha utokeaji na utendaji wa tendo. Kyeu (2011) anasema kitendoneni ni kujaribu kutekeleza jukumu fulani kwa kunena. Nadharia ya kitendoneni inahusishwa na John Langshaw Austin, (1962), kupitia kwa mihadhara yake aliyotoa na ikachapishwa baadaye na kuitwa “Jinsi ya kutenda kwa kutumia maneno.” Nadharia aliyoanzisha imekuwa ikiendelezwa na wasomi mbalimbali kama vile Searle, (1975), De Pietro, (1994), na Resani,

(2014). Austin (keshatajwa) anaeleza kwamba, kwa kutamka neno, kuna uwezekano wa tendo kutekelezwa papo hapo kama inavyoelezwa katika kauli yake kuu ya, "tunalofanya tukitamka neno." *(TY)* Katika kauli hii, inadhihirika kuwa, utamkaji wa neno husababisha utendaji wa jambo. Kyeu (2011) anadai kwamba Austin alianzisha nadharia hii kupinga mawazo ya wanafalsafa na wanaisimu wa mwanzo ambao mawazo yao yalikuwa kwamba kazi ya lugha ni kueleza, kufafanua, na kuarifu mambo mbalimbali.

Kulingana na Austin (ashatajwa), si mara zote lugha hutumiwa kufafanua mambo bali mara nyingine hutumika kutenda. Anarejelea lugha hii kama lughatendi ama matamkotendi ambayo Searle (1975) anayaita matendoneni. Austin, (1962: 101-107), anasema kitendoneni kimejengwa kwa mihimili mitatu ambayo ni:

i. ***Tendo la kutamka**:* Ni kile kisemwacho na jinsi kinasemwa. Tendo la kutamka ni utoaji au uwasilishaji wa maneno yenye uamilifu ndani yake, yaani, maneno yanayotolewa yawe na maana.

ii. ***Lengo au dhamira ya kutamka**:* Tamko linapotolewa, hutupa nia au kusudio la tamko hilo. Kwa Searle, tamko lina nguvu fulani zinazolifanya kuwa na uwezo wa kutenda au kuathiri hisia za msikilizaji na kubadilisha tabia zake na hali yake kwa ujumla.

iii. ***Matokeo au athari za tamko**:* Athari ya tamko kwa msikilizaji hutokana na mwitiko wake kutokana na tamko lililotolewa. Kwa mfano, kuomba msamaha kwa msikilizaji kunaonyesha kuwa tamko la mnenaji limemwathiri msikilizaji kwa kumfanya atambue kuwa amekosea. Vilevile, kitendo cha kuridhia au kutoridhia kwa anayeombwa msamaha kinadhihirisha athari ya tamko hilo.

Mhimili wa kwanza ulitusaidia kubainisha matamko yaliyotamkwa katika usimulizi na jinsi yalitamkwa. Mhimili wa pili ulituongoza kubainisha dhamira ya kutamka matamko yaliyotamkwa, na mhimili wa tatu ulitusaidia kubainisha athari za matamko kwa wasikilizaji.

Austin (Ashatajwa) anagawa vitendoneni katika aina sita ambazo ni; kitendoneni cha maamuzi, kitendoneni cha maagano, kitendoneni cha maagizo, kitendoneni cha hisia, kitendoneni cha maelezo na kitendoneni cha hulka. Yeye Searle (1975) anaainisha vitendoneni kwa kuzingatia kigezo cha athari ya kitendoneni. Hata hivyo, mawazo yao hayatofautiani. Ni misamiati tofauti tu wanayotumia kuainisha vitendoneni. Kwa mfano, pale ambapo Austin anakiita kitendoneni cha maamuzi, Searle anakiita kitendoneni cha msimamo, na msimamo unatokana na uamuzi unaofanywa. Vilevile, pale ambapo Austin anakiita kitendoneni cha maagizo, Searle anakiita kitendoneni agizi. Maana inabaki ileile ikiwasilishwa na maumbo tofauti ya istilahi.

Resani (2014) alihakiki hali zinazosababisha kufaulu kwa kitendoneni kama zilivyotolewa na Austin, (1962). Kutokana na uhakiki wake, aligundua kwamba kutokea na kufaulu kwa kitendoneni kunategemea kuwepo kwa masharti yauatayo:

**Hadhi na Mamlaka ya Mnenaji**
Mnenaji awe wa hadhi ya juu na mwenye mamlaka kuliko msikilizaji. Hoja hii inasisitizwa na Di Pietro (1987) anaposema kuwa utoaji wa kitendoneni unaendana na mahusiano ya kijamii na hadhi ya kila mtu ili hisia kugusiwa.

*1. Mpokeaji awe Muafaka*
Ili kutokea tendo, msikilizaji awe muafaka ili aweze kulitenda tendo aliloambiwa. Kwa mfano, katika tamko lifuatalo; "*Nimekufukuza shuleni kwanzia saa hii kwa sababu ya tabia yako ya kutorokatoroka shuleni,*" mwanafunzi awe ni yule aliyetoroka shuleni.

2. *Hadhi na Mamlaka ya Msikilizaji*

Utekelezaji wa tamko pia hutegemea hadhi ya msikilizaji. Ikiwa mnenaji ni wa hadhi ya juu kuliko msikilizaji, tamko lake litazingatiwa na msikilizaji

3. *Wakati Muafaka wa Tamko*

Tamko, wakati mwingine, hutegemea mazingira na wakati ambapo limetolewa. Hivyo, hadhira hutekeleza tamko kulingana na wakati. Kwa mfano, mhadhiri akisema, "*Kila mmoja wenu ajitayarishe kuwasilisha makala yake kesho kuanzia saa sita adhuhuri*", ni dhahiri kwamba haya ni mazingira ya chuoni na wakati maalumu ambapo wanafunzi watakuwa darasani kuwasilisha makala. Kwa hiyo tamko hilo litakubalika.

4. *Kuwepo kwa Maleba*

Hii huhusisha vifaa na mavazi maalumu ambayo huendana na tukio maalum lipate kueleweka. Yanaweza kuwa mavazi ya kitamaduni, ya kijeshi, au vifaa vingine kama mikuki au bakora.

5. *Kuwepo kwa Lengo*

Kitendoneni kinakubalika iwapo lengo la tamko linadhihirika wazi kwa msikilizaji na ikiwa utekelezaji wake si mgumu. Hii ina maana kwamba tamko linapaswa kuwa na manufaa kwa msikilizaji. Kwa mfano, katika tamko, "*Mfalme wa Buganda ameamrisha Waganda wote kuweka bidii katika sekta ya kilimo ili kudumisha chakula*", wasikilizaji wote hawana budi kutekeleza tamko hilo kwa sababu lengo la tamko hilo litawafaa wote.

Mawazo ya Resani yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa yalituongoza kubainisha ufaafu wa vitendoneni vilivyotamkwa. Hata hivyo, mawazo yake yanahitaji kuchunguzwa zaidi ili kubainisha miktadha na hali mbalimbali zinazostahili kuwepo ili kitendoneni kufaulu, yaani, masharti haya yanafaa ikiwa wanajamii wote ni watiifu wanaofuata utaratibu uliopo. Kwa mfano, tukirejelea masharti matatu ya kwanza; Hadhi na Mamlaka ya Mnenaji, Mpokeaji awe muafaka na adhi na mamlaka ya msikilizaji mfululizo, tuligundua kwamba masharti haya yana mapungufu kwa sababu hayakuzingatia wanajamii wanaokiuka mienendo na kaida za jamii yao.

**Mbinu za Utafiti**

Data ilikusanywa nyanjani na muundo wake ulikuwa wa kithamano ambapo mwelekeo wa uchanganuzi ulikuwa wa kiufafanuzi na kimaelezo.

Utafiti wenyewe ulifanyika Magharibi ya Kusini mwa Uganda katika jimbo la Ankole katika vijiji vya wilaya tatu za Ibanda, Mbarara na Sheema. Wilaya hizi zinatambulika kuwa zina wabobezi wengi wa fasihi simulizi ya Kinyankole.

Utafiti ulihusisha watafitiwa 36 wa miaka 60-86 kwa sababu ya tajriba yao kuhusu usimulizi wa ngano za Kinyankole. Walitutolea maarifa kuhusu mitindo ya usimulizi wa ngano na jinsi usimulizi huo uliathiri wasikilizaji.

Tuliteua watafitiwa kwa kutumia sampuli za aina mbili; sampuli kusudio na sampuli mkufu. Katika sampuli kusudio, tulihoji watafitiwa wenye umri wa miaka 60-86 kwa sababu ya ujuzi wao kuhusu ngano za Kinyankole. Hawa, tuliwafikia kwa kuongozwa na wenyekiti wa vijiji tulivyotembelea. Wakati ambapo mwenyekiti hakuwa na muda, alitupa mwanakijiji mwingine ambaye aliandamana nasi kuelekea kwa mtafitiwa mwingine. Wakati ambapo mwanakijiji aliyetuongoza alitingwa na shughuli na kushindwa kuendelea nasi, tulitumia sampuli mkufu ambapo mtafitiwa tuliyefikia kwanza alituelekeza kwa mtafitiwa mwingine hadi tulipofikia wa mwisho.

Tulipata data ya utafiti wetu kutoka kwa watafitiwa 36 ambao tuliteua kimaksudi. Tuliteua watafitiwa 12 kutoka kila wilaya. Idadi hii ilitosha kutupa data tuliyohitaji.

Data ya utafiti huu ni vitendoneni ambavyo vilijitokeza katika ngano saba za Kinyankole, ambazo tuliteua kimaksudi kutoka kwa ishirini tulizokusanya nyanjani. Ngano hizi ni:

1. *Nyabwangu na Nyabucureera* (Dada wawili; *Nyabwangu* na dadake *Nyabucureera*)
2. *Mungure na Nyamaziga* (Ndugu wawili; *Mungure* na dadake *Nyamaziga*)
3. *Kijumbe n'Akafunzi* (Kijumbe na kidege; *Kijumbe* na kidege kinachoitwa *Akafunzi*)
4. *Miyanda* (Kijana wa kiume anayeitwa *Miyanda*)
5. *Rwooma Rurumbaire na Bwiisho Burintenda* (Ndugu wawili; *Rwooma Rurumbaire* na kaka yake *Bwiisho Burintenda*)
6. *Kishokye ky'omwishwa tohunga sho?* (*Kishokye ky'omwishwa*, kimbia babako)
7. *Zeebiikiire n'Orukooko* (Mwanamume mmoja kwa jina la *Zeebiikiire* na jinyama linalojulikana katika Kinyankole kama *Orukooko*)

Tulibainisha vitendoneni vilivyotamkwa katika usimulizi wa ngano na baada ya kivichanganua tukabainisha malengo ya kuvitamka na matokeo ya utamkaji.

Ili kupata data ya utafiti, tulitumia mbinu ya mahojiano na uchunguzi hirikishi. Mahojiano yalitusaidia kupata data ya msingi kama Kothari (2004) anavyobainisha kwamba mahojiano hurahisisha upatikanaji wa data kwa kuwa yanawajumuisha wanaojua kusoma na wasiojua kusoma. Kothari anaeleza kwamba mbinu hii humpa fursa mtafiti kuuliza maswali ya ziada kutokana na majibu anayotolewa na watafitiwa. Tuliweza kuuliza maswali ya ziada ambayo yaliibuka kutoka kwa majibu tuliyotolewa.

Aidha, tulitumia mbinu ya uchunguzi shirikishi ambapo tilijumuika na vikundi vya watafitiwa na kuchukua nafasi sawa na wanavikundi hivyo na kushiriki kikamilifu kama wao katika kuitikia masimulizi. Tuliwatembelea wasimulizi nyumbani kwao au mahali pao pa kazi na kuwaomba kushiriki katika mchakato wa kusimuliana ngano. Mtafiti alishiriki kama msikilizaji wa kuitikia masimulizi huku akitazama kwa makini miondoko na mihemko ya wasikilizaji na ya msimulizi mwenyewe. Baada ya kila ngano, tuliuliza maswali kuhusu ngano hiyo.

Data tuliyokusanya tulichanganua kwa mujibu wa Nadharia ya Kitendoneni na malengo ya utafiti. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari.

**Vitendoneni katika ngano za Kinyankole**
Katika uchambuzi wa vitendoneni, tulifuata mwainisho wa vitendoneni kulingana na Austin, (1962), ifuatavyo:

***Kitendoneni cha Maamuzi***
Austin (1962) anaeleza kuwa mnenaji katika kitendoneni hiki anaweza kufanya maamuzi ya mwisho au yasiyo ya mwisho na maamuzi hayo yanaweza kumwathiri yeye mwenyewe au msikilizaji kwa njia chanya au hasi. Mara nyingi, maamuzi yanayofikiwa na mnenaji huathiri msikilizaji. Katika ngano za Kinyankole, kulijitokeza vitendoneni kadhaa vya maamuzi. Mathalani katika ngano ya *Nyabwangu na Nyabucureera*, mhusika Nyabwangu anaamua kumfuata Nyabucureera kwenye mlima ambao watu wanaogopa kupanda. Mamake anamkataza asimfuate Nyabucureera lakini anakaidi na kwenda. Anamwambia mamake:

*1. Nyowe nakugira ngu ninza kuzayo!*
***Tafsiri:*** *Mimi nimekwambia, nitaenda huko! (TY)*

Kitendoneni katika kauli hii ni, *ninza kuzayo (nitaenda)*. Lengo la kitendoneni hiki ni kuonyesha maamuzi ambayo Nyabwangu amefanya. Nyabwangu ameamua kwenda licha ya kuagizwa na mamake kutoenda. Tamko la Nyabwangu linamwathiri mamake kwa njia hasi kwa sababu ya

madharau na ukaidi wa mtoto wake. Kitendo cha Nyabwangu cha kukaidi maagizo ya mamake kinapinga mawazo ya Resani (2014) katika masharti aliyopendekeza katika nadharia ya kitendoneni kwamba, kwa kitendoneni kufaulu; hadhi na mamlaka ya mnenaji yawe ya juu kuliko ya msikilizaji; mpokeaji awe muafaka; hadhi na mamlaka ya msikilizaji yawe ya chini kuliko ya mnenaji. Katika kitendoneni hiki, hadhi na mamlaka ya Nyabwangu (msemaji) ni ya chini kuliko ya mamake (msikilizaji). Mbali na hayo, kitendoneni kilifaulu kwa sababu mnenaji (Nyabwangu) aliendа licha ya kwamba msikilizaji (mama) hakuridhia maamuzi yaliyofanywa na mnenaji. Vilevile, lengo la kitendoneni lilikuwa linaeleweka; kumzuia kupanda mlima ili asifikiwe na matatizo. Hata hivyo, yeye alikataa katakata akakaidi maonyo yaliyokuwa katika kitendoneni. Katika hali ya kinyume kama hiyo, Resani anasema, mnenaji anaweza kuathirika kuliko msikilizaji kama inavyodhihirishwa na maafa yaliyomfikia Nyabwangu ya kuolewa na mbwa.

Hali kama hii imejitokeza pia katika ngano ya *Rwooma Rurumbaire na Bwiisho Burintenda,* ambapo Rwooma Rurumbaire, almaarufu Rwooma anakaidi maagizo ya babake ambaye anamwagiza kurudi nyumbani akaolewe. Rwooma anakataa kwa kuwa ameshafanya uamuzi wake kwamba hataolewa hadi atimize lengo lake la kuolewa na mwanamume atakayelipa ng'ombe wengi. Uamuzi wake unadhihirika katika maneno anayotuma kwa babake:

2. *…gyenda ogambire taata, oti aziteere igyende, we takenzire kushweerwa...*
**Tafsiri:** *Nenda kamwambie baba, eti warudishe ng'ombe wao, yeye hataki kuolewa… (TY)*

Vitendoneni katika kauli hii ni *aziteere igyende* (awapige ng'ombe waende) na *takenzire kushweerwa* (bado hataki kuolewa). Nia ya vitendoneni hivi ni kuonesha uamuzi wa Rwooma wa kutoolewa hadi atakapojiamulia. Athari ya kitendo cha Rwooma cha kukataa kuolewa kinamwathiri mamake wa kambo na babake kwa kuwakosesha mali waliyohitaji. Ingawa babake anajaribu kumlazimisha kuolewa, Rwooma anashikilia uamuzi wake hadi aitimize ndoto yake ya kulipwa mahari anayotaka. Kulingana na masharti ya kitendoneni kama yalivyotolewa na Resani (2014), hadhi na mamlaka ya mnenaji (Rwooma) ni ya chini kuliko ya msikilizaji (mzazi). Hata hivyo, kitendoneni kilitendeka, yaani, Rwooma alikataa kuolewa. Hali hii inabainisha udhaifu wa masharti ya Resani kwa kuonyesha kuwa kitendoneni kilitendeka licha ya mnenaji kuwa wa hadhi ya chini kuliko msikilizaji.

***Kitendoneni cha Maagizo***

Austin (1962) anaeleza kwamba mnenaji katika kitendoneni cha maagizo huwa anamwagiza msikilizaji kutekeleza jambo alilomwagiza. Kufaulu kwa kitendoneni cha maagizo hutegemea sana mnenaji kuwa mwenye hadhi ya juu kuliko msikilizaji kama ilivyopendekezwa na Resani (2014). Kulingana na ufafanuzi wa Resani, ni dhahiri kwamba msikilizaji asipotenda alichoagizwa, mnenaji anaweza kutenda jambo au msikilizaji anaweza kuhasirika. Vitendoneni vya aina hii vilijitokeza katika ngano kadhaa, kwa mfano, *Nyabwangu na Nyabucureera*, *Kishokye ky'omwishwa tohunga sho? Na Zeebiikiire N'orukooko.*

Katika ngano ya *Nyabwangu na Nyabucureera*, Nyabwangu anajiamulia kufuata Nyabucureera ambaye ametumwa kwa mfalme. Mfalme anaishi nyuma ya mlima mrefu sana ambao haujawahi kupandwa na mtu yeyote. Huu ndio mlima ambao Nyabwangu ameamua kupanda ili awahi kwa mfalme kabla Nyabucureera hajafika. Mamake anamwagiza:

3. *Otakigyeza kusharabamba orushozi orwo! Nooha oworareebire narutemba?*
**Tafsiri:** *Usithubutu kupanda mlima huo! Umewahi kumwona nani akiupanda?*

Kitendoneni katika tamko hili ni *otakigyeza kusharabamba* (*usithubutu kupanda*). Lengo la kitendoneni hiki ni kumwagiza Nyabwangu kutopanda mlima ambao ni hatari kuupanda. Nyabwangu alikaidi agizo la mamake na kuupanda mlima huo.

Katika ngano ya *Kishokye ky'omwishwa tohunga sho,* baba alipoteza mkewe na akaamua kuoa mwingine. Mke huyo alimtolea maagizo kabla hajamwoa. Alimwagiza kuua mtotowe ndipo amwoe. Anaagiza:

4. *Waza kunshweera, obanze oite omwaana waawe!*
**Tafsiri:** *Kabla hujanioa, ua mtoto wako kwanza!*

Lengo la kitendoneni hiki ni kuonesha maagizao ya mwanamke kwa mwanamume. Tamko la mwanamke linawaathiri watu kadhaa; baba ambaye anaitikia kwa kutenda kitendo cha kuua mtoto wake, mtoto ambaye anauawa na wanajamii ambao wanashuhudia kisa. Kama nadharia ya kitendoneni inavyosisitiza, tamko limetamkwa likasababisha kitendo cha kukata mtoto kichwa. Katika ngano ile ile, mwanamke anaendelea kuagiza:

5. *…kandi ku oramwite, ondetere omutwe gwe!*
**Tafsiri:** *…na baada ya kumwua, uniletee kichwa chake! (TY)*

Lengo la kitendoneni hiki ni kuonesha agizo la mwanamke na jinsi mwanamume anaitikia agizo hilo. Anaitikia agizo hilo kwa kukata mtotowe kichwa. Kama Resani (2014) anavyopendekeza kuwa kwa kitendoneni kufaulu, mnenaji awe wa hadhi ya juu kuliko msikilizaji. Mwanamke katika muktadha huu ndiye wa hadhi ya juu kwa sababu mwanamume ni mhitaji. Hivyo, kitendoneni kinafaulu kwa vile mwanamume anatekeleza alichoagizwa kwa kumkata mtotowe kichwa. Athari ya kitendoneni hiki ni kwamba mwanamume alikata kichwa cha mtotowe na kukipelekea mkewe.

Katika ngano ya *Zeebiikiire n'Orukooko,* jinyama linamwagiza Zebiikiire:

6. *…okwateho omwana wawe omwe, omutemateme omuteeke, kundaije nshange enyama zahiire. Wahurira?*
**Tafsiri: …** *chagua mtoto wako mmoja, umkatekate, umpike ili nikirudi, nipate nyama zimeivai. Umesikia?*

Katika kauli hiyo, vitendoneni ni *okwateho omwaana wawe omwe (chagua mtoto wako mmoja)* na *omutemateme omuteeke (umkatekate umpike)*. Lengo la vitendoneni hivi ni kulazimisha Zeebiikiire kuchinja mtoto wake na kupika nyama yake. Kwa vile hadhi ya jinyama ni ya juu na ya Zebiikiire ni ya chini, Zeebiikiire hana budi kutenda alichoagizwa. Kwa kuegemea nadharia ya kitendoneni, tumetambua kwamba jinyama limetamka na Zeebiikiire anaitikia kwa kutenda. Kitendoneni hiki kinamwathiri Zeebiikiire kwa kumhuzunisha akifikiria jinsi atakavyomchinja mtoto wake.

***Kitendoneni cha Maagano***
Austin (1962) anafafanua kwamba kitendoneni cha maagano huhitaji watu kuwekeana agano ambalo sharti litimizwe. Maagano ni ya aina mbili; kuafikiana na mtu mwingine au kutakiana heri mnapoachana.

Katika ngano ya *Miyanda,* mbwa wa Miyanda, baada ya kuzeeka, anaona atakufa. Kwa hiyo anaagana na Miyanda:

7. *…kundaabe naafiire, oije ombagye, onyihemu omutima, ogukariirire, oguhanike omukisasi. Kwokuba waguhanikiremu, tihariho ekirikwiita.*
**Tafsiri:** *…nitakapofariki, nichinje, utoe moyo wangu, uuchome, uuanike katika paa, juu ya mlango. Utakapouanika humo, hakuna kitakachokuua. (TY)*

Vitendoneni katika kauli hiyo ni, *oije ombagye (unichinje), onyihemu omutima (utoe moyo wangu), ogukaririre (uuchome),* na *oguhanikye omukisasi (uuweke katika paa la nyumba).* Lengo la vitendoneni hivi ni kumwelekeza Miyanda kuishi maisha yasiyo na usumbufu. Katika muktadha wa vitendonen hivi, hadhi ya mnenaji (mbwa) ni ya juu kuliko ya msikilizaji (Miyanda). Hivyo, Miyanda analazimika kutenda kama alivyoelekezwa na mbwa wake. Athari za vitendoneni hivi ni kwamba Miyanda alihuzunika kwa kifo cha mbwa wake na pia alitekeleza aliyoambiwa na mbwa.

Katika ngano ya *Rwooma Rurumbaire na Bwiisho Burintenda*, mama wa kambo anafanya agano na watoto wake wa kambo kwamba hatarudia kuwatesa bali atawatunza ifaavyo. Anasema:

8. *Kandi nindaganisa kureeberera Bwiisho ogu nk'okukirikwetengyesa…*
**Tafsiri:** *Naahidi kumtunza Bwiisho huyu kama inavyotakikana*

Kitendoneni katika tamko hili ni *nindaganisa kureeberera Bwiisho (Naahidi kumtunza Bwiisho).* Lengo la kitendoneni hiki ni kuonesha jinsi mama wa kambo ameathirika na kuahidi kumtunza Bwiisho. Matokeo ya kitendoneni hiki ni kwamba walishawishika na ndio maana walikubali kuishi kwa furaha. Aidha, kuna kubadilika kitabia kwa mama wa kambo ambaye anaapa kutowanyanyasa. Hoja hii imejengeka kwa mhimili wa pili wa nadharia ya kitendoneni unaoangazia athari za kitendoneni kwa msikilizaji. Austin (1962) anasema vitendoneni vya maagano hulenga kuwekea mwathiriwa vikwazo ili kumzuia kufikiwa na matatizo au hasara. Mama wa kambo amewekewa vikwazo vya kutorudia kumnyanyasa Bwiisho.

Aidha kuna vitendoneni vya maagano vya kutakiana heri watu wanapotengana. Pengine, mmoja anaweza kuwa anakabiliwa na mauti na akaamua kuagana na jamaa zake kama ilivyo katika ngano ya *Mungure na Nyamaziga***.** Katika ngano hiyo, Mungure anaanguka katika kina kirefu ambapo hawezi kutoka. Kwa hiyo, anaamua kuagana na dadake, kwa kumtolea maneno ya mwisho:

9. *Nyowe tindaija, Nyamaziga maawe…*
**Tafsiri:** *Mimi sitarudi tena, Nyamaziga mama…*

Kitendoneni katika kauli hii ni *nyowe tindaija (Mimi sitarudi tena).* Nia ya kitendoneni hiki ni kumuaga Nyamaziga. Kitendoneni hiki kinamwathiri Nyamaziga kihisia kwa kumhuzunisha sana akaangua kilio.

***Kitendoneni cha Hisia***

Austin (1962) anasema kwamba katika kitendoneni cha hisia, mnenaji hutamka maneno ambayo yanagusa hisia za msikilizaji. Anaeleza kuwa matokeo ya athari za vitendoneni vya hisia huwa ni hali kama; mihemuko, furaha, huzuni, wasiwasi, majuto na nyingine. Katika usimulizi wa ngano za Kinyankole, vitendoneni vya hisia vilidhihirika katika ngano kadhaa kama vile, *Mungure na Nyamaziga* na *Kishokye Ky'omwishwa tohunga sho?*

Katika ngano ya *Mungure na Nyamaziga,* Mungure alianguka katika kina kirefu sana huku akiwinda. Hangeweza kutoka, maana angefia humo. Baada ya Nyamaziga kugundua kwamba kakake ameanguka humo, anaenda kwenye kina kumpa buriani kabla hajafa. Anapofika, anamwita kwa huzuni na wanasikilizana kwa mbali sana kwa sababu ya urefu wa kina. Wanaagana kupitia wimbo wanaoimbiana:

10. *Kundaabe naafiire, Nyamaziga maawe*
*Omukazi wangye omugarure owaabo, Nyamaziga maawe.*

**Tafsiri:** *Nitakapoaga, Nyamaziga mama*
*Mke wangu umrudishe kwao, Nyamaziga mama. (TY)*

Tamko, *kundaabe nafiire (nitakapoaga)* linamtayarisha Nyamaziga kusikiliza agano analokaribia kupewa na kakake. Agano hili linapatikana katika kitendoneni, *omukazi wangye omugarure owaabo (mke wangu umrudishe kwao).* Nia ya kitendoneni hiki ni kumwelekeza Nyamaziga atakavyoshughulikia mke wa Mungure baada ya Mungure kufariki. Matamko haya yanamhuzunisha Nyamaziga na analia sana. Pia anatenda kama alivyoagana na kakake kwa kurudisha Bi. Arusi kwao.

***Kitendoneni cha Maelezo***

Katika kitendoneni hiki, mnenaji hutoa maelezo kwa watu au kutoa uthibitisho wa jambo fulani (Austin, 1962). Lengo la vitendoneni vya maelezo ni kuifanya hadhira ielewe hali ilivyo. Vitendoneni vya aina hii vilijitokeza sana katika ngano za Kinyankole, kwa mfano, *Zeebiikiire N'orukooko*, *Rwooma Rurumbaire na Bwiisho Burintenda* na *Nyabwangu na Nyabucureera*.

Katika ngano ya *Zeebiikiire n'Orukooko,* jinyama linaporudi kutoka mawindoni, linakuta watu katika nyumba yake wakionekana dhaifu. Baada ya kuwaamkua, linawaambia:

11. *Nareeba ngu mwine enjara. Mwihure enyama murye, mubyame, mutuure nanye.*

**Tafsiri:** *Nimetambua mna njaa. Pakueni nyama mkale, mkimaliza mlale, muishi nami.*

Katika kauli hii, kitendoneni *Nareeba ngu mwine enjara (Nimetambua mna njaa)* kinatoa uthibitisho wa kuwapo kwa kitendoneni *mwihure enyama murye (pakueni nyama mkale).* Kitendo cha kupakua nyama kula kimesababishwa na hali ya kuwa na njaa. Hali hii inashabihiana na maelezo ya nadharia ya kitendoneni kwamba tamko linapotamkwa, msikilizaji anaathirika na anaitikia kwa kutenda jambo. Kwa msingi huo, familia ya Zeebiikiire haikuwa na budi kuitika kwa kupika nyama iliyotarajiwa na jinyama. Isingekuwa kwa mke wa Zeebiikiire kutafakari na kutafuta nyama nyingine, Zeebiikiire angemchinja mtoto wake. Kama Resani (2014) anavyoeleza, kufaulu kwa kitendoneni kunamhitaji mnenaji kuwa wa hadhi na mamlaka ya juu kuliko msikilizaji. Kwa hiyo Zeebiikiire alitenda kwa kuwa jinyama ni lenye nguvu kuliko yeye. Hata hivyo, sharti hili lina mapungufu. Kwa mfano, tuliona Nyabwangu katika ngano ya *Nyabwangu na Nyabucureera* akikataa kutenda aliyoambiwa na mamake ambaye ni mwenye nguvu. Katika ngano ya *Rwooma Rurumbaire na Bwisho Burintenda,* Rwooma anakataa maagizo ya mamake wa kambo ambaye ni mwenye hadhi na mamlaka ya juu. Kwa hoja hii, tunaweza kuhitimisha kwamba ufanisi wa kitendoneni pia hutegemea nia ya mnenaji na tabia za msikilizaji.

***Kitendoneni cha Hulka***

Kulinganan na Austin (1962), kitendoneni cha hulka kinahusiana na tabia za kijamii. Kinahusu mwitiko wa mtu kuendana na kitu ambacho mwingine amekifanya. Kwa mfano;

Katika ngano ya *Rwooma Rurumbaire na Bwisho Burintenda,* Rwooma anatamka maneno ambayo yanamwathiri mama wa kambo na kumchochea kuomba msamaha. Rwooma anatamka;

12. *Muka tata akatunyangaraza ekirikumara. Nimushaba atagaruka kunyangaraza munyanyazi…*

**Tafsiri:** *Mama yetu wa kambo alitunyanyasa vya kutosha. Namuomba asirudie kunyanyasa kaka yangu…*

Kitendoneni katika kauli hii ni *nimushaba atagaruka kunyangaraza munyanyazi… (namuomba asirudie kunyanyasa kaka yangu…)* Nia ya kitendoneni hiki ni kumzuia mama wa kambo asirudie kumnyanyasa Bwiisho. Athari za kitendoneni hiki ni kwamba mama wa kambo anaitikia kwa kuomba msamaha. Kuomba msamaha kwa mama wa kambo kumetokana na tahadhari ya Rwooma kwake. Kihalisia, Rwooma ni mwenye hadhi ya chini kwa vile ni binti lakini muktadha wa kitendoneni hiki unamchora kuwa ndiye wa hadhi ya juu kwa sababu ndiye mwenye ng'ombe

ambao mama wa kambo anahitaji. Kwa hiyo, mama wa kambo hana budi kutenda alichoambiwa na bintiye wa kambo. Baada ya Rwooma kumtahadharisha, mama wa kambo anatamka:

> 13. *Ninshaba omwishiki wangye kunsasira ebinakukozire…*
> ***Tafsiri:*** *Nakuomba binti yangu kunisamehe yote niliyokutendea…*

Kitendoneni katika kauli hii ni *ninshaba kunsasira (naomba unisamehe)*. Kitendo cha mama wa kambo cha kuomba msamaha kimetokana na matamko makali ya Rwooma. Rwooma anapoathirika na kukiri kwamba amemsamehe. Anasema;

> 14. *Nyowe naamusasira, kwonka niimushaba, atagaruka kubonabonesa munyanyazi…*
> ***Tafsiri:*** *Nimemsamehe lakini namwomba asirudie kunyanyasa kaka yangu…*

Kitendoneni, *naamusasira (nimemsamehe)* kinanuia kubainisha maridhiano ambayo yamefikiwa na kitendoneni *atagaruka kubonabonesa munyanyazi* (asirudie kunyanyasa kakangu) kinalenga kumwekea kikwazo mama wa kambo cha kutorudia kunyanyasa Bwiisho ikiwa maridhiano yao yatadumu. Athari za vitendoneni hivi ni kwamba Rwooma anagusika na kumsamehe mama wa kambo na mama wa kambo anaahidi kutomnyanyasa Bwiisho tena.

**Hitimisho**

Utafiti umehitimisha kwamba usimulizi wa ngano za Kinyankole ulitumia mitindo kadhaa ya kisanaa na mitindo hiyo ilitumia vitendoneni ambavyo viliathiri hadhira kwa njia chanya au hasi. Athari hizi zilidhihirika katika vitendo ambavyo wasikilizaji walitenda kutokana na vilitendoneni vilivyotamkwa. Mifano ya athari chanya ambazo ziliibuliwa na vitendoneni vilivyotamkwa ni kama vile; furaha, vicheko na kuunga mkono baadhi ya vitendo vilivyotendwa katika ngano. Athari hasi ambazo zilidhihirika ni kama, huzuni, chuki na hasira ambazo zilisababisha vilio, vifo na ulipizaji kisasi.

## Marejeleo

Austin, J. L. (1962). *How to do things with Words*. Oxford University Press.

Di Pietro, R. J. (1987). *Strategic Interaction: Learning Languages through Scenarios*. Cambridge University Press.

Finnegan, R. (1974). *How oral is Oral Literature?* Bulletin of the School of Oriental and African Studies, University of London.

Insaidoo, K. A. (2011). *Moral Lessons in African folktales.* Author House.

Kirindi, G. N. P. (2008). *History and Culture of the Kingdom of Ankole.* Fountain Publishers.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques* (Second Revised Edition). New Age International (P) Ltd.

Kyeu, D. (2011). *Nadharia ya Kitendoneni na Jinsi Inavyoweza Kutumika Kuchanganua Usemi.* Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madson.

Kyobutungi, J. T. (2012). *Fire Place Experience in Ankole*. Bishop Stuart University.

Mahmoud, Y. H. (2018). *Vitendoneni katika hotuba za kampeni za uchaguzi za mwaka 2015, na athari zake kwa wanajamii wa Zanzibar.* Utafiti wa uzamiifu, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). (Haujachapishwa).

Matinde, R. S. (2012). *Daphina ya lugha, isimu na nadharia: kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.* Serengeti Educational Publishers Ltd.

Mwene Mushanga, T. (1969) *Folk Tales from Ankole.* Milton Obote Foundation

Nganwa, K. K. (1962). *Emitwarize ya Wakami*, Fountain Publishers.

Ninsiima, M. (2021). *The Potential of Kinyankore Culture as a tourism product*. Nkumba University Press.

Okpewho, I. (1986). The Study of African Oral Literature. *Présence Africaine*, *139*, 20–40. http://www.jstor.org/stable/24351122
Resani, M. (2014). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Karjamer Publishers
Searle, J. R. (1975). *Speech Acts: An Essay in Philosophy of Language.* Cambridge University Press.